Sudan Kusini

Mwongozo wa Mwalimu

# Kiswahili 4

**Kiswahili kwa kidato cha Nne(4)** kimeandikwa na wizara ya Elimu na Mafunzo kwa jumla, Ikishirikiana na wataalam wa lugha.

Kitabu hiki kinamwelimisha mwanafunzi kwa mazoezi na vitendo.

**Kila darasa linajumuisha Kitabu cha Mwanafunzi na Mwongozo wa Mwalimu.**

**Kila Kitabu cha mwanafunzi kinakupa:**

- Ufafanuzi mwafaka wa mtaala wa kitaifa.
- Msingi bora katika kiswahili.
- Uwasilishaji na ufafanuzi wa hoja unazotakiwa kujifunza.
- Mazoezi mwafaka yanayoonyesha jinsi Kiswahili Kinaweza kutumika katika mifano halisi maishani.
- Fursa ya ushirikiano kupitia kwa kazi ya vikundi.
- Michoro ya kusisimua.

**Masomo yote katika mfululizo huu wa msingi yalitengenezwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mkuu, Jamhuri ya Sudan Kusini.**

**Vitabu vimeundwa kutekeleza somo la shule za msingi,na wakati huo huo kuwawezesha wanafunzi na ujuzi unaofaa katika jamii ya kisasa ya kimataifa**

**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kitabu kitakachopatikana kikiuzwa kwa njia yoyote kitatawaliwa na muuzaji kuchukuliwa hatua za kisheria.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

Sudan Kusini

Mwongozo wa Mwalimu

# Kiswahili 4

Kidato cha Nne



**Kitabu hiki ni Mali ya Wizara ya Elimu na Mafunzo.**

**Kitabu hiki hakiruhusiwi kuuzwa.**

**Kimefadhiliwa na:**

GLOBAL PARTNERSHIP for EDUCATION
quality education for all children

# Jinsi ya kutunza kitabu chako.

**Mambo muhimu ya kuzingatia.**

1. Unaombwa kuhakikisha umenawa mikono kabla ya kukitumia kitabu chako.
2. Tumia kalamu ya rangi kuonyesha kazi iliyofanywa.Usikunje karatasi za vitabu.
3. Kitabu kikiharibika,hakikisha kinakarabatiwa kwa haraka.
4. Kuwa mwangalifu wakati unapomwazimu mwenzako kitabu.
5. Tafadhali kiweke kitabu chako mahali pakavu na pasipokuwa na unyevu.
6. Unapokipoteza kitabu chako, mjulishe mwalimu wako.

**Mambo unayokatazwa kufanya.**

1. Usiandike ndani au juu ya kitabu chako.
2. Usikate michoro iliyokitabuni.
3. Usirarue kurasa zozote kitabuni.
4. Usikiache kitabu kikiwa kimefunguliwa.
5. Usikiweke kitabu chako kwenye mkoba uliojazwa vitabu zaidi.
6. Usikitumie kitabu chako kujifunika wakati wa mvua.
7. Usikikalie kitabu chako.

Sudan Kusini

KIDATO CHA
4

# Kiswahili

*Mwongozo wa Mwalimu*

© 2018, THE REPUBLIC OF SOUTH SUDAN, MINISTRY OF GENERAL EDUCATION AND INSTRUCTION. All rights reserved. No part of this book may be reproduced by any means graphic, electronic, mechanical, photocopying, taping, storage and retrieval system without prior written permission of the Copyright Holder. Pictures, illustrations and links to third party websites are provided in good faith, for information and education purposes only

Ilifadhiliwa na:

Kitabu hiki ni Mali ya Wizara
Kimetadhiliwa na: ya Elimu na Mafunzo.

**KITABU HIKI HAKIRUHUSIWI KUUZWA.**

# FOREWORD

I am delighted to present to you this Teacher's Guide, which is developed by the Ministry of General Education and Instruction based on the new South Sudan National Curriculum. The National Curriculum is a learner-centered curriculum that aims to meet the needs and aspirations of the new nation. In particular, it aims to develop (a) Good citizens; (b) successful lifelong learners; (c) creative, active and productive individuals; and (d) Environmentally responsible members of our society. This textbook, like many others, has been designed to contribute to achievement of these noble aims. It has been revised thoroughly by our Subject Panels, is deemed to be fit for the purpose and has been recommended to me for approval. Therefore, I hereby grant my approval. This Teacher's Guide shall be used to facilitate learning for learners in all schools of the Republic of South Sudan, except international schools, with effect from 4th February, 2019.

I am deeply grateful to the staff of the Ministry of General Education and Instruction, especially Mr Michael Lopuke Lotyam Longolio, the Undersecretary of the Ministry, the staff of the Curriculum Development Centre, under the supervision of Mr Omot Okony Olok, the Director General for Quality Assurance and Standards, the Subject Panelists, the Curriculum Foundation (UK), under the able leadership of Dr Brian Male, for providing professional guidance throughout the process of the development of National Curriculum, school textbooks and Teachers' Guides for the Republic of South Sudan since 2013. I wish to thank UNICEF South Sudan for managing the project funded by the Global Partnership in Education so well and funding the development of the National Curriculum, the new textbooks and Teachers' Guides. I am equally grateful for the support provided by Mr Tony Calderbank, the former Country Director of the British Council, South Sudan; Sir Richard Arden, Senior Education Advisor of DfID, South Sudan. I thank Longhorn and Mountain Top publishers in Kenya for working closely with the Ministry, the Subject Panels, UNICEF and the Curriculum Foundation UK to write the new textbooks. Finally, I thank the former Ministers of Education, Hon. Joseph Ukel Abango and Hon. Dr John Gai Nyuot Yoh, for supporting me, in my role as the Undersecretary, to lead the Technical Committee to develop and complete the consultations on the new National Curriculum Framework by 29 November 2013.

The Ministry of General Education and Instruction, Republic of South Sudan, is most grateful to all these key stakeholders for their overwhelming support to the design and development of this historic South Sudan National Curriculum. This historic reform in South Sudan's education system is intended to benefit the people of South Sudan, especially the children and youth and the future generations. It shall enhance the quality of education in the country to promote peace, justice, liberty and prosperity for all. I urge all Teachers to put this textbook to good use.

May God bless South Sudan. May He help our Teachers to inspire, educate and transform the lives of all the children and youth of South Sudan.



Deng Deng Hoc Yai, (Hon.)
Minister of General Education and Instruction, Republic of South Sudan

# YALIYOMO

SURA YA 1: MAAMUZI YA MAISHA NA MATATIZO YA KIJAMII ................................ 1

SURA YA 2: USAWA WA JINSIA .................. 9

SURA YA 3: UHUSIANO WA KIMATAIFA13

SURA YA 4: UTALII.................................... 17

SURA YA 5: IMANI NA TAMADUNI .......... 21

SURA YA 6: HAKI ZA BINADAMU ........... 23

# SURA YA 1: MAAMUZI YA MAISHA NA MATATIZO YA KIJAMII

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**SHAIRI A:**

**HAKIBA HII MWAFAKA: MAJIBU**

1. Pesa/dirahimu
2. Ujumbe katika ubeti wa 2 ni kuwa pesa itakuondolea shida.
3. Ubeti wanne unasema tuacha ufukara na tuwe imara.
4. Dhamira ya mshairi ni kuekeza pesa maana zitakufaidi baadaye.
5. Maudhui yanayojitokeza katika shairi ni kuwajibika maishani kwa kuwekeza pesa.

**SHAIRI B:**

**USIFE MOYO**

1. Msomaji anahimiza juu ya kuwa na moyo wa kutenda jambo japo wengi watamchekelea.
2. Ubeti wa 2 unamlenga mwanafunzi na ujumbe ni afanye bidii masomoni.
3. Dhana ya Misri kulingana na ubeti wa 4 ni umaskini.
4. Anayelengwa ubeti wa 5 ana shida ya kukosa mpenzi.
5. Dhamira ya mshairi ni kujizatiti kwa kila jambo.

**Shairi C:**

**SUBIRA HUVUTA HERI**

1. Mshairi anashukuru kwa nia gani katika ubeti wa 1?
2. Kulingana na shairi lawama utoka kwa sababu ya kutovumilia.
3. Faida za kusoma ni kuvuna mazuri na faida za elimu.
4. Muumini anashauriwa amutumikie Mungu kwa uaminifu na atapata baraka.

5. ujumbe wa ubeti wa 5 ni kwa yule anayetafuta kazi.Anaambiwa amwamini Mungu na atajaliwa.

## KUSOMA

**KIFUNGU A**

**MAJIBU**

1. Baadhi ya watu huamini kuwa hatima ya mtu maishani huwa imepangwa kabla hajazaliwa.
2. Hatima ni hali ya maisha ya mtu ambayo mtu anajiamulia.
3. Baadhi ya watu katika dunia ya leo wanaamini wanapaswa kuponda mali kwani hatima yao inajulikana na Mungu.
4. Mafikira ya kutofanya chochote maishani imewaathiri sana vijana na wanaishi katika ufukara.
5. Wao hushiriki chochote eti kwa kuwa tayari wamejaaliwa kesho yao.
6. Hawana haja na elimu. Wanaamini eti shuleni ni pahali pa kungojea utamu wa
7. Kuchochea migomo,kutumia dawa za kulevya ,starehe zisizo na mipango ,kushiriki ngono kiholelaholela
8. Wengine ni majambazi sugu. Wao hushirikiana na wavunja sheria sugu kupora mali ya wenyewe bila mtu kuwashuku.
9. kuwapigiga,kuwafanyisha kazi ya sulubu hata vitendo vya ngono
10. Huvaa nguo fupi,wanavaa nguo zisizo na maadili nguo ambazo ni nyepesi zinazoonesha nguo za ndani au vitopu na vimini zinazoacha sehemu kubwa ya maungo yao nje wenyewe wanajiita masista duu.Wengine hutia herini chungu nzima masikioni  na kujipaka rangi za kutisha mdomoni.
11. Huwafurahisha daima kwa darahima/pesa kochokocho.
12. Wanazuzuliwa na hizo ngori zao nyeupe pepepe na kufanya juu chini kusaka ngwenje kokote zinakopatikana ili kujinunulia vipodozi aina aina vya kubadili ngozi zao.
13. Ndio.wametoboa masikio na kuvaa hereni, wamesuka nywele na kupaka poda sura zao pia kuvaa suruali chini ya makaliona wo .Wanavaa mikufu

inayong’ara kuliko ile ya kina dada. Nayo mitindo ya nguo huzihangaisha akili zao kutwa kucha. Macho na masikio yao hukaa chonjo kila dakika ili wafahamu ni mitindo ipi mipya iliyoingia hasa kutoka ng’ambo

14. Marafiki wabaya.
15. wanaiga mambo yasiyofaa kupitia mitandao ya kijamii
16. Ujana ni moshi tu.
17. Kwa kujifunga masombo /kujikaza kwa majukumu ya baadaye. Ni kipindi cha kujitafutia maarifa tunu/kochokocho.
18. Wazazi ,Viongozi mbalimbali
19. Baadhi ya vijana kudharau na kutoziheshimu mila na desturi zao.
20. Kuwa na heshima.

**KIFUNGU B**

## WOSIA KWA VIJANA NA WAZAZI

**MAJIBU**

1. Waache kuona ugumu kwenye kila matatizo na tuaanze kuona fursa
2. Dira/mwelekeo ya taifa lolote ipo mikononi mwao
3. Itakuwa ni upotevu wa rasilimali
4. kusoma, kuandika, kudadavua/pata suluhisho la tatizo na kuzungumzia maslahi ya taifa
5. wenye kutoka nje ya mipaka ya utulivu
6. madaktari, wajasiriamali, wanasayansi ,marais
7. Kwa kukusanya uchafu kutoka nyumba kwa nyumba
8. Nitaonekana , watu wengine watanionaje nisipofanikiwa
9. Kulelewa kwa kuonyeshwa kila kitu mpaka wazazi au walezi wakuruhusu, hata kubadilisha nguo utotoni ilikuwa mpaka umuulize mlezi au mkubwa wako.
10. kwetu sisi maskini, mimi sijasoma, mimi siwezi, mimi kwetu hatujafanikiwa
11. Maumivu hutujenga kuwa watu wapya
12. Mtoto wakoanapoelekea katika rika laujana na kepuvuka.

13. Hofu yako kubwa ni, hujui mtoto wako atatumia njia gani kukwepa mitego ya jamiina kama ataingia kwenye mtego na kunaswa atatokaje?
14. Kuchota tabia za wengine.
15. Mtoto kushikilia usia waliopewawa juu ya mambo ya maisha na wazazi wao,
16. Mzazi kujisikia aibu ya kukaa naye chini na kumpa mtotpwe ukweli wa mambo ulivyo
17. Mtoto anaachiwa jukumu la awe na uzoefu binafsi wa kutambua vita iliyo mbele yake ni ya namna gani na vipi ataishinda
18. vyombo vya habari au uzoefu atakaokutana na yeye mwenyewe
19. masuala ya uzazi, mimba za utotoni, na utoaji wa mimba
20. mtaani,shule au hata vyuoni
21. Hawakupata taarifa sahihi kutoka kwa wazazi wao juu ya madhara ya tabia hizo,na pia kukwepa kuonekana mshamba.
22. ajueitamsaidiaje katika maisha yake ya kujitegemea
23. ili wapate nafasi ya kufanya shughuli zao wenyewe
24. Atumia busara zako kumuunganishana na wana familia wengine
25. Vijana hawaoni tabu kubadilisha marafiki mara kwa mara.
26. Kujaribu kumuongoza njia sahihi za mahusiano.
27. Kumfundisha mambo yapi yana umuhimu na yapi hayana umuhimu kwake katika mtandao
28. Kuwa na tafsiri tofauti tofauti juu ya maana halisi ya kufanikiwa katika maisha.
29. Mpe usalama,muonyesha upendo na kumjali,weka misingi yako ambayo yeye ataifuata kipindi yupo chini yako,muadhibu pale inapobidi,kuwa na muda wa kutosha kukaa naye na kuzungumza naye,fuatilia uhusiano wake na wengine,muonyeshe mfano.
30. Kwa kuanza kumtegenezea mazingira hayo tangu mapema utaweza kujivunia tabia yake ya kesho.

**KIFUNGU C**

## UAMUZI MAISHANI

**MAJIBU**

1. Kuchagua kitu katikati ya vitu vingi ambavyo vinatuchanganya akili.
2. Kuanza na kimoja na kumalizia na vingine.
3. Hatua ya kudaka kitu inahusishakuzifanyia kazi fursa nafasihaupaswi kukaa tu.
4. Baada ya kuamua unataka kitu nafasi zinaweza kupitia marafiki zako, wafanyakazi wenzako, au kupitia matangazo uliyoyafanya maeneo mbalimbali
5. Mwandishi anaposema lazima ufungue macho unapokitaka kitu anamaanisha uwe unaangalia nafasi zikitokea.
6. Kulingana na kifungu uzinduzi ni tendo la kuchukua na kuuendelea na mkondo uliouchagua ili ukutoe kimaisha.
7. Siogope kupata hasara katika chochote ufanyacho maana kupitia hasara tunajifunza mbinu bora zaidi za kuitafuta faida kubwa.
8. Glasi iliyo tupu inatunza katika maisha unakutegemea wewe, ikiwa unataka kujaza maisha yako na lawama au na shukrani.
9. Mwandishi anasema kama maisha yako ni ya kujutia utajutia kozi unayosoma, kazi unayofanya, biashara unayofanya, mke au mume mliyeoana nae, watoto uliowazaa
10. Maamuzi ya mtu mwenye maaadili ya kidini ni tofauti na maamuzi ya yule asiye na dini.
11. Mapito magumu yanatunza kustahimili kesho,
12. Maisha ya binadamu yanategemea maamuzi anayoyafanya kila siku.
13. Yako yale yatakupelekea kufanikiwa na yapo maamuzi ukiyafanya yanakupelekea moja kwa moja kwenye kushindwa.
14. maamuzi uliyoyafanya wewe siku za nyuma
15. Uliyiojifunza utawakwamua wengi watakao kwama katika tope linalo fanana na lakwako kesho.
16. Amua kuwa makini na kile unachokizingatia.

17. kupoteza muda, kutojisomea, kutokujiwekea malengo
18. Atakufanya uendelee na kuwa mshindi katika maisha yako.
19. Wale tu ambao maisha yao wameamua kuwekeza kwa hali na mali.
20. Mwanafunzi atoe maoni yake, mwalimu hakiki hoja za mwanafunzi.

**KIFUNGU D**

## KUKATA TAMAA

**MAJIBU**

1. Ni hali ya kufikia kikomo juu ya mafanikio ya jambo halisi,nihali ya kuchoshwa au kuvunjwa moyo kunakotokana na mtazamo hasi
2. Hali ya kukata tamaa hutokea katika hali ambalomtu amepoteza wazo au matumaini ya kufanikiwa katika matarajio yake ya kupata kitu fulani au kufanikiwa kwa jambo lolote alilopanga kulifanya.
3. Nyumbani, Kazini, shuleni, kwenye biashara, katika mahusiano au mahali pengine popote katika mfumo wa maisha.
4. Dalili za kukata tamaa hutofautina kulingana namazingira, sababu, wahusika, matukio na wengineyo. Taja aina mbili za dalili za kukata tamaa.
5. Dalili ambazo watu wengine nje ya mhusika hawawezi kuzitambua kiurahisi, ni muhusika tu ndiye anaweza kuzitambua au kuhisi.
6. Dalili za nje ni dalili ambazo watu wengine nje ya mhusika tunaweza kuwa mashahidi kwa kuziona kwa uwazi na kutambua kwamba mwenzetu amekata tamaa.
7. Msukumo wa mawazo ni ushawishi wa mawazo.
8. Dalili ya kuchoka kimawazo inadhihirika kupitia ikiwa mawazo yako yamechoshwa kwa kuliwazia jambo fulani ambalo mwanzoni ulikuwa umelipanga vizuri au kila mtu unamwona kama mzigo kwako.
9. Mawazo hasi huleta woga wa kufanya jambo kwa kuhofia kushindwa au kukosa uhakika wa kufikia malengo.
10. Unapolemeza ubongo wakokufikiria unaKukosa ubunifu wa njia mbadala.

11. Dalili ya kukosa furaha kama njia ya kukata tamaa ina dalili zingine kama kutofurahia ushauri na maamuzi ya haraka.
12. Mtu anaposihisi hafai anajilaumu kuwa maisha yake hayana jambo lolote la maana la kuchangia na huyafai kabisa, anahisiana hatia nyingi.
13. Maneno ya mtu yanaweza kuonyesha kukata tamaa ikiwa anatumia maneno yanayokiri kushindwa.
14. Utovu wa nidhamu unaoshiria kukata tamaa ni kama utumiaji wa dawa ya kulevya na ukahaba.
15. Mabadiliko ya tabia yanayoonyesha kukata tamaa ni toka tabia nzuri kwenda tabia mbaya?
16. Dalili ya kukata tamaa kwa kujitenga huandamana na kukosafuraha,kuwa mnyonge, juhudi zake hupungua
17. Wanapokumbuka mambo magumu waliyopitia.
18. Hii ni dalili ya kukata tamaa, waliumizwa mioyo na watu wenginewanapoelezea juu ya matukio yaliyowaumiza,
19. Kutofikia malengo uliyojiwekea, Kubaki na hali yeyote ambayokablaulihitajikujikwamua. Mfanoumaskini, maradhi, ujinga KuchanganyikiwakiakilinauwezowakokiutendajI
20. Shinikizo la damu, madonda ya tumbo,kisukari.

## SARUFI

### VIUNGANISHI

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutamua maana ya viunganishi katika lugha ya Kiswahili.
2. Wanafunzi wataje aina na zifa za viunganishi.
3. Wanafunzi watunge sentensi sahihi wakitumia aina tofauti za viunganishi.
4. Wanafunzi wakamilishe mazoezi katika vutabu vyao.
5. Mwalimu ahakiki majibu ya wanafunzi.

### Zoezi

**A. Tambua viunganishi katika sentensi hizi.**

1. Alimbeba **ijapo** kwa shida.

2. Mwandikie barua **angalau** tujue iwapo alifika.
3. Chukua jembe, kisu **pamoja na** kifyeko.
4. Nimesafiri kwa ndege **sembuse** gari moshi.
5. **Lau** tungekubaliana, matatizo hayangetokea.
6. Alimpakulia chakula, **isitoshe** akampa malazi.
7. Atatrudi kesho **kwa minajili** ya kukuomba msamaha.
8. **Aidha** uchukue vifaa vyote **au** uachane navyo.
9. Simjui **wala** simdhamini.
10. Watafika kwa sherehe **muradi** usiwaitishe zawadi.

**B. Unganisha sentensi zifuatazo kwa kutumia viunganishi sahihi.**

1. Lopi ni mwalimu pia mkulima.
2. Sitafika hospitali kumwona lakini nitamtuma kakangu.
3. Michezo ya raidha hujumuisha mbio pamoja na ujenzi wa viungo vya mwili.
4. Sokoni kumejaa matunda mengi kama vile maembe, tikitimaji, machungwa na fenesi.
5. Ningelijua, nisingelienda kwake.
6. Jikakamue kwa masomo kwa sababu maisha ni kujitegemea.
7. Yote nilimtendea lakini hakunishukuru.

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi andike kisa juu ya njia za kujipa matumaini maishani.
2. Mwanafunzi andike mazungumzo juu ya mwathiriwa wa dawa za kulevya na mhudumu wa akili.Mwalimu hakiki kazi ya mwanafunzi.Insha iwe na muundo wa mazungumzo.
3. Mwanafunzi ajadili vile Vijana wanaweza kujiendeleza kwa nyanja mbalimbali.insha ichukue muundo wa mjadala.

# SURA YA 2: USAWA WA JINSIA

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**SHAIRI:**

1. Mshairi anaongea juu ya mtoto wa kiume.
2. Mhusika wa anayetajwa atatandikwe kwa sababu amechelewa kufika nyumbani.
3. Anayezungumziwa aulizwe matumizi ya pesa, ikiwa amelipa madeni aelezee mabaki yako wapi, ikiwa ni dawa aeleze ni za pesa gapi.
4. Mzazi anaonywa juu ya malezi ya mtoto wa kiume.anambiwa amlea kwa usawa kama wa kike.
5. Mshairi anatufunza juu ya usawa wa jinsia.

## KUSOMA

**KIFUNGU A:**
**MAJIBU**

1. Taja majukumu ya mwanamke wa Sudan kusini ni kuleta jamii pamoja. Kusaidia majirani na familia za waathirika wa mgogoro, kuongoza majadiliano kati ya jamii ili kukuza uponyaji na uaminifu.
2. Rais wa sudan kusini naongoza kwa kupigania kuheshimu kwa haki za wa wanawake, anasisitiza kutupiliwa mbali kwa mila na tamaduni potovu.
3. Wasichana wadogo wanadhulumiwa kupitia kuolewa mapema, wanapigwa, kutolewa maneno machafu na kutishiwa kuwa wao ni mkosi au kupelekwa polisi ili kuwalazimisha kuolewa.
4. Ni nini nia ya kuwaoza wasichana mapema?a kuwafurahisha wasichana wao na familia zao,ni njia muhimu kwa familia hizo kujipatia utajiri
5. k.uweka sheria za ambazo zinatoa umuhimu katika kulinda kuwaoza watoto na wanawake ,kwa kutumia njia mbadala za kupata elimu kwa wasichana, wakinamama na watu wengine waliopata ujauzito

6. Zinakwamisha maendeleo ya kijamii, kielimu, kiuchumi, kiafya na usalama wa wanawake na wasichana wadogo katika familia na jamii zao.
7. wanaume kutoka vikundi vya kupigana ndio waliongoza mazungumzo ya meza ya amani
8. Huduma mbili muhimu zinahitajika na wanake sudan kusini ni upatikanaji wa afya na elimu,.
9. Wanawake wajawazito wanaseka kwa vile wanakaa kwenye hofu ya usalamavipi?
10. Wauguzi wanahitajika kuwawaliofundishwa.

**KIFUNGU B**

**MAJIBU**

1. Makabila ya Sudan Kusini yanatofotiana kwa kuwa kila mmoja ikiwa na utamaduni wake wa kipekee.
2. Usambasaji wa makabila haya hutegemea maeneo ya kijiografia.
3. Waume wa kuoa huchanguliwa vipi sudan kusini?
4. Wanawake wa Sudan Kusini hawana majukumu ya mamlaka au umuhimu wowote ulioheshimiwa katika familia zao au jamii. Wajibu wao ni wa kuolewa
5. Wao huolewa na mtu aliyechaguliwa na familia nje ya mfumo wa mahari, mfumo unaohusisha wanawake kama bidhaa ya kununuliwa au kuuzwa.
6. Dinka na Nuer.
7. Wakimbizi wengi walienda Uganda na Kenya, na pia katika ulimwengu wa magharibi.
8. Mkataba mkuu wa  Amani ulifanyika Nairobi, Kenyaw
9. Mkataba mkuu wa Amani ulilenga kukomesha vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa miaka miwili kati ya kaskazini na kusini mwa Sudan.
10. Matokeo mazuri ya elimu kwao wenyewe, watoto wao, na familia zao na waligundua tamaduni ambazo mwanamke hakutaka kulazimishwa katika ndoa.

11. Mwanamke wa kijijini ametwikwa kuangalia kwa watoto na wazee wa familia iliyopanuliwa, kutoa huduma zote za maisha ya nyumbani na ya kila siku, na kusimamia uzalishaji wa chakula.
12. Ndio.
13. Elimu itasaidia aje jamii ya watu wa sudan kusini?
14. Mwanamke aliyesoma uboresha kijamii kiuchumi na maisha ya familia.
15. Kufundishwa kuwa utaalamu wao katika fani mbalimbali utachangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya vijiji na maeneo ya mijini.

## SARUFI

### USEMI HALISI NA USEMI WA TAARIFA

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutofautisha kati ya usemi halisi na usemi wa taarifa.
2. Wanafunzi wajijumuishe katika kuzitambua sifa za usemi halisi na zile za usemi wa taarifa.
3. Mwalimu awaongoze wanafunsi katika kujibu maswali.
4. Mwalimu ahakiki majibu ya wanafunzi.

### Zoezi

**A. Sahihisha sentensi zifuatazo katika usemi halisi.**

1. Asha alimwambia rafike kwamba angemtembelea jioni iliofuata.
2. Mwalimu mkuu alisema kwamba ikiwa kuna mwanafunzi ambaye hakuwa amepata vitabu aende amuone.
3. Mununuzi alisisitiza kwamba ubee bidhaa kwani bei ilikuwa imepunguzwa.
4. Juma, Sarah,Deng, Rosa na Awel, ni washiriki walioambiwa na mhubiri wangemuona baada ya ibada.
5. Mtoto alimlilia mamake akitaka chakula.

**B. Andika sentensi katika usemi wa kauli halisi.**

1. Mwanasiasa aliahidi wananchi, “Nitawaletea maji ya mfereji na matangi ya kuhifadhi maji.”

2. Fundi wa viatu alimaka, “Mimi hushona viatu sio nguo!”
3. Mlezi aliwaeleza watoto, “Kesho tuataenda kutembelea mbuga ya wanyama pori.”
4. Askari alimwita habusu, “Nassa! Nassa! Nassa! Sitakuonya tena.”
5. Wavulana walisema, “Tunataka usawa baina yetu na aasichana.”
6. “Salaale! Kwa nini unamtusi mwenzako hivyo?” Kijana alimaka.
7. Mwalimu mkuu alisema, “Kesho sitaruhusu mwanafunzi kuhudhuria masomobila kumleta mzazi wake kwanza.”
8. “Susana! Susana! Nakuita mara ngapi? Sisi tunaondoka leo,” Maria alisema.

## ZOEZI

**Majibu:**

1. Mwanafunzi alikiri kwamba, angefurahi sana, angeupita mtihani huo.
2. Wanafunzi walikiri ya kwamba wao walipenda kusoma.
3. Kaka aliniahidi kwamba angeninunulia mkoba.
4. Asha  alieleza kuwa mjomba alikuwa amewatembelea.
5. Nyanya aliwaonya wajukuu wake kwamba asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

## KUANDIKA

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika uandishi wa insha. Ahakiki insha za wanafunzi.

1. Andika kisa kuhusu nafasi ya mwanamke katika jamii.
2. Kuelimisha mwanamke ni kuelimisha jamii. Jadili.
3. Andika mazungumzo kuhusu amani kati ya mwalimu na afisa wa polisi.

# SURA YA 3: UHUSIANO WA KIMATAIFA

## KUSIKILIZ NA KUZUNGUMZA

1. Mwalimu awaongoze wa kuzungumzia umuhimu wa uhusiano wa kimataifa.
2. Wanafunzi wazungumzie manufaa ya mataifa kuwa na uhusiano mwema.
3. Wanafunzi watoe maoni yao kuhusu jinsi chi ya Sudan Kusini inaweza kuimarisha uhusiano wake na mataifa mengine ya ulimwengu.
4. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuzungumzia mchango wa matifa mengine katika kuinuka kwa nchi ya Sudan Kusini.

## MAJIBU

1. Tendo la kihistoria lilitendeka Ikulu Jijini Dar es Salaam.
2. Tendo hili ni la kihistoria kwa sababu rais John Pombe Magufulina Rais Salva Kiir Mayarditwalisaini Mkataba wa kuiwezesha Jamhuri ya Sudan Kusini kuwa Mwanachama kamili wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
3. Ni rais wawili waliokuwapo.
4. Rais John Pombe Magufulina Rais Salva Kiir Mayardit.
5. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na  Sudan Kusini
6. Taja tarehe za matukio yafuatayo yaSudan kusini :
    a) Kupata uhuru-09 Julai, 2011.
    b) Kuwasilisha maombi yao ya kujiunga na jumuiya-10 Novemba, 2011.
    c) Kukubaliwa kwa ombi-Machi 2016.
    d) IKutia saini makubaliano-15 Aprili, 2016
7. Tukio hili la kihistoria kutokea wakati Tanzania ikiwa ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika MasharikI.
8. Sudan kusini imekuwa ikishirikiana na nchi zingine kwa nyanja za tamaduni, ushirikiano wa kibiashara na uchumi na ukaribu wa kijografia
9. Sudan kusini imeshaanza kufanyia mabadiliko mifumo mbalimbali kwenye Serikali ili kuweza kushiriki kikamilifu katika hatua mbalimbali za mtangamano ikiwemo kuunda Wizara inayoshughulikia masuala ya Afrika Mashariki.

10. Ndio. Makubalianoyaliafikiwa kuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki itashirikiana kwa karibu na Jumuiya ya Kimataifa kuhakikisha wananchi wa Sudan Kusini waliothirika na migogoro na kuikimbia nchi zingine watarejea kwa ajili ya kuendeleza nchi yao.

**KIFUNGU B**

**KUSIKILIZ NA KUZUNGUMZA**

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi kuchambua maana ya hotuba.
2. Wanafunzi waisome hotuba iliyovitabuni mwao.
3. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuzungumzia mambo yanayozingatiwa wakati wa kuandika hotuba.

## 1. Insha ya Hotuba

Hotuba ni ujumbe unaopitishwa na yule anayetarajiwa kuupitisha. Katika hotuba, hatibu huzingatia mambo kadhaa, kama vile:

1. Hadhira itakayomsikiliza- Je, ni wazee au vijana wamejumuika pamoja?
2. Mazingira atakayotolea hotuba yake.
3. Kipimo cha hotuba yake (ili isiwendefu sana au fupi sana). Hotuba inapaswa kuwa ya wastani.
4. Hotuba ilenge mada husika bila kwenda nje ya kilichotarajiwa kuwasilishwa. Hotuba lazima:

(I) Kitambue cheo cha waliohudhuria kutoka juu hadi chini.

(ii) Iwasilishwe kwa njia inayoeleweka na wanaoisikiliza.

(iii) Itumie nafsi ya kwanza,ya pili au ya tatu.

(iv) Itumie wakati uliopo.

(v) Imalizike kwa kuwashukuru waliohudhuria.

(vi) Iwe na kichwa

Kichwa cha hotuba lazima kiwe na yafuatayo:

1. Neno ‘hotuba’.

2. Anayehutubu.

3. Wakati wa hotuba.

4. Mahali pa hotuba.

5. Atakayesoma hotuba.

Mfano wa hotuba, kitabu cha mwanafunzi ku. 47/48

## 2. Insha ya kumbukumbu

Insha hii anahusu taarifa ya mambo ambayo yalifanyika katika mkutano fulani. Insha ya kumbukumbu huzingatia mambo yafuatayo:

1. Kichwa cha kumbukumbu za mkutano husika. Kichwa hubeba:

a) Jina la chama au kikundi kinachokutana.
b) Mahali mkutano uliandaliwa
c) Tarehe na wakati wa kufanyika kwa mkutano huo.
d) Saa za kuanza mkutano huo.

Mwalimu awaongoze wanafunzi kuandika yafuatayo:

i. jina rasmi la kikundi kinachokutana.

ii. Mahali panapoandaliwa mkutano husika.

iii. Tarehe ya kufanyika mkutano.

iv. Wakati wa kufanyika mkutano.

## SARUFI

**VIREJESHI ‘O’ NA ‘AMBA’**

1. Mwalimu awaeleze wanafunzi matumizi ya O-rejseshi na amba.
2. Wanafunzi wasome sentensi katika umoja na wingi kubainisha matumizi ya virejeshi hivi katika ngeli tofauti.
3. Wanafunzi wakamilishe zoezi katika vitabu vyao.
4. Mwalimu ahakiki majibu ya wanafunzi.

### Zoezi

**Rekebisha virejeshi ‘O’ na ‘amba’ katika sentensi zifuatazo.**

1. Kiberiti kinachotumiwa ni chetu.
2. Msumari ambao ulipigiliwa umetoka.
3. Mashati yanayofuliwa yataanikwa.
4. Chai inazomwagika imechemka.
5. Maabara yanayofagiliwa yatatumiwa.
6. Bawabu ambaye anafunga mlango ni mkubwa.
7. Mkutubu anayetupatia vitabu amepotea.
8. Udhaifu unaomkumba unamlemaza.
9. Kukimbia ambako alifanya kulimnusuru.
10. Kondeni mnamofyekwa ni mzuri.

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi andike insha juu ya faida za muungano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.
2. Mwanafunzi ajadili kwa kutoa hoja za kuunga na kupinga na baadaye atoe msimamo wake.
3. Msimamo wa mwanafunzi udhihirike kupitia hoja zake.

# SURA YA 4: UTALII

## KUSOMA

### KIFUNGU A

### UTALII

1. Ni hali ya kusafiri huku na huko kuyafurahia mandhari. Pia kule kushughulikia watalii au kuwahudumia ni Utalii.
2. Kutembea kutoka mahali pamoja hadi pengine katika nchi yako, na kuna kutoka nchi moja hadi nyengine.
3. Watalii wengi huwa wanvutiwa na wanyama wa porini, pwani vitu vya kihistoria, mila na utamaduni na hata mazingira.
4. Miti huleta mvua. Kwa hivyo utunzaji wa mazingira unasaidia pakubwa kuongeza idadi ya mvua katika sehemu mbalimbali nchini. Zaidi ya hayo, miti huwa chakula na mahali pakuishi pa wanyama wengi.
5. Huwekeza katika sekta mbalimbali nchini, hulipa ushuru mwingi na hivyo basi kuimarisha uchumi wa nchi.
6. Kuwaonyesha wenzao wanaporudi nyumbani. Hii huwapa wengine hamu ya kutembelea nchi wanazoziona kwenye picha na hivyo kuongeza idadi ya watalii nchini.
7. Idadi ya watalii inavyoongezeka, ndivyo mapato kutokana na utalii yanavyozidi kuongezeka.
8. Kwa mujibu wa taarifa, Sekta ya utalii iko kwa kiwango cha chini.
9. Uwanja wa Kimataifa wa Juba, ambao ndio uwanja mkubwa nchini Sudan Kusini, umepanuka kutoka kuwa wa ndege za kawaida hadi ndege za kimataifa ambazo zinafanya kazi ya usafiri.
10. Hifadhi ya Taifa ya Bandingilo, Hifadhi ya Taifa ya Lantoto, Hifadhi ya Taifa ya Nimule, Hifadhi ya Taifa ya Shambe na Hifadhi ya Taifa ya Taifa. Ez Zeraf Game Reserve, Ashana Game Reserve, Reserve ya Bengangai, Bire Kpatuos Hifadhi ya Hifadhi, Hifadhi ya Hifadhi ya Chelkou, Hifadhi ya Mbuga Fanikang, Hifadhi ya Mbuga ya Juba, Hifadhi ya Mbuga ya Kidepo, Hifadhi ya Visiwa vya Mbarizunga, na Hifadhi ya Nyaraka ya Numatina
11. Eneo la ndege wa kuvutia ni Sudd,
12. Eneo hili liko na idadi ya ndege aina 400.

13. Mataifa yanayorudisha nyuma utalii wa Sudan Kusini ni Marekani, Canada na Uingereza.
14. Marekani inaonya wananchi wake dhidi ya kutembelea Sudan Kusini kutokana na migogoro ya silaha iliyoendelea nchini.
15. ukosefu wa miundombinu kwa ajili ya utalii na vita vya wenyewe kwa wenyewe.

**KIFUNGU B**

## UTALII TANZANIA

1. Utalii ni moja kati ya sekta zinazoingiza kipato kikubwa kwa taifa la Tanzania kwa kipindi kikubwa.
2. Nchi hii imejaliwa rasilmali halisia nyingi ikiwemo mito mikubwa na midogo, mabonde na milima
3. Mbega, vyula, kima, nyani, tumbili, vinyonga, viboko, mamba.
4. Katavi, Mikumi, Ngorongoro, Serengeti, Manyara, Tarangire, Selou, Ruhaa, Mkomanzi, Kitulo na nyinginezo ndogondogo.
5. Tanzania inavivutio vingi ambayo mataifa mengi Afrika na kwingineko duniani hawana.
6. Maporoko ya Kalambo, Ndola waterfalls na Irente view.
7. Mapato ya nchi hii yanayotokana na utalii ni duni sana yakilinganishwa na nchi jirani ya Kenya.
8. Vivutio vya utalii vya Tanzania havitangazwi; Nchi ya Tanzania ina ukosefu wa mabandiko na matangazo yanayoonyesha vivutio kwenye miji na maelekezo yanayoonyesha vivutio vingine vilivyopo kwenye miji ya jirani. Hii inaathiri sana ubora wa kuwajuvya watalii juu ya vivutio nchini. Jambo jingine ni kuwa mabasi ya abiria toka Dar es Salaam kwenda mikoani na nchi jirani hayana vipindi vya kutangaza utalii, hata yale yanayovuka mipaka kwenda nchi jirani yanashughulika na filamu za kigeni kama Kichina, Kihindi hata filamu zinazoonyesha utalii.
9. Kenya wanatangaza vya kwao mara 12 zaidi kuliko Tanzania.
10. Tafiti mbalimbali za nchi zilizofanikiwa kiutalii duniani zinaonyesha kuwa vivutio vya utalii vinavyotangazwa zaidi ndivyo huleta watalii wengi zaidi na hivyo kuingiza fedha nyingi zaidi.

11. Hii inaathiri sana ubora wa kuwajuvya watalii juu ya vivutio nchini.
12. Mabasi ya abiria toka Dar es Salaam kwenda mikoani na nchi jirani hayana vipindi vya kutangaza utalii, hata yale yanayovuka mipaka kwenda nchi jirani yanashughulika na filamu za kigeni kama Kichina, Kihindi hata filamu zinazoonyesha utalii.
13. Wao pia wangeweza kutangaza utajiri wa nchi hii kwa kuweka filamu zinazoonyesha milima, mabonde, mito, mbuga na kila kilichopo na maelekezo yake kwa lugha ya msafiri kama vile Kiingereza, Kifaransa, Kijerumani, Kichina na kadhalika.
14. Watalii wanalalamikia kukosekana kwa usafiri wa ndege nchini Tanzania.
15. Kwa sehemu kubwa watalii wanaotembelea Tanzania wanahudumiwa na magari ya kukodisha yaliyosajiliwa na usajili wa nchi za nje kama Kenya au Afrika Kusini yakiwapeleka kutembelea vivutio nchini humo.
16. Kuna uchache wa huduma ya usafiri wa anga kutoka mahali pamoja hadi pengine, wakati wote wa siku, hali inayoonekana kuathiri utalii.
17. Ukosefu wa maji safi, huduma za afya na hoteli au vyumba vya kulala.
18. Kwa sasa kila mahali utakuta ugali, wali na nyama tu. Nchi ya Tanzania inahitajika kuwa na chakula cha kienyeji kinachowaovutia watalii ilikuepushe tabia ya wao kuja na vyakula na vitu vingine toka wanakotoka.
19. Je nchi ya Tanzania inaweza kubali hali yake ya utalii? Thibitisha kwa hoja tatu.
20. Utalii una umuhimu sana katika kukuza uchumi wan chi yoyote ile.

## SARUFI

### UUNDAJI WA NOMINO

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutambua vitenzi vyenye asili ya kibantu na vile vyenye asili ya kigeni.
2. Wanfunzi wataje baadhi ya vitenzi wakitambulisha asili yake.
3. Mwalimu awaongoze wanafunzi kayika kukamilisha zoezi la uundaji wa nomino kutokana na vitenzi vya kigeni.
4. Mwalimu ahakiki majibu ya wanafunzi.

**Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo.**

1. Zuru -
2. Fariji - faraja
3. Kashifu - kashfa
4. Uza -
5. Hubiri - mhubiri
6. Dharau -
7. Dhuru -
8. abudu - ibada
9. hukumu - hakimu
10. ahidi - ahadi

## KUANDIKA

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika unadishi wa insha.
2. Wanafunzi wajibu maswali ya insha wakizingatia maagizo.

# SURA YA 5: IMANI NA TAMADUNI

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuzungumzia tamaduni mablimbali. Wanafunzi wazitaje baadhi ya tamaduni wazijuazo pamoja na zile ambazo wamepata kushiriki. Wanafunzi wajivunie imani na tamaduni zao.

## KUSOMA

### MAJIBU

1. Watu wengi hupenda kufikiria utamaduni ni vitu ambavyo tunavyoviona kama mapishi, mavazi, ngoma, muziki, kama desturi ya sherehe.
2. Maana ya utamaduni kulingana na aya ya kwanza. Utamaduni ni jinsi binadamu anavyokabili maisha katika mazingira yake
3. Njia tatu zinazotumiwa kuelezea utamaduni.Kama maonjo ya hali ya juu katika sanaa, kama utamaduni wa juu,na kama Mkusanyiko wa maarifa ya binadamu.
4. Kwa sababu utamaduni kazi zote afanyazo mwanadamu na namna anavyokabiliana na mazingira yanayomzunguka ili kukidhi mahitaji yake muhimu ya kumwezesha kuishi. Mahitaji hayo muhimu ni chakula, makazi na mavazi
5. Maana ya methali ‘mkataa kwao ni mtumwa’.una maana kwamba, mtu ambaye anadharau maisha na tamaduni ambazo amekulia nazo, ametekwa kimawazo na yuko tayari.
6. Lugha hunasa muhimu wa desturi ya jamii fulani. Kutokana na lugha, unafahamu dhana yake ya msingi juu ya mtu binafsi jinsi wanavyohusiana kwa vikundi, matarajio ya jamii, sherehe za jadi
7. Ni pale ambapo kila kundi la utamaduni linadhani njia yao ni sahihi, ni “maarifa ya kawaida” tu ambayo inapaswa kila mtu ajue.
8. Ngazi za kikabila, ngazi ya mtu binafsi, ngazi ya kati ya kimapenzi mahusiano.

9. Mgogoro wa vita, ubaguzi wa rangi na kunyanyasa wengine talaka na huzuni.
10. La,wengine wanaona miko na makatazo katika mila na tamaduni zetu kuwa imepitwa na wakati au haikupaswa kuwepo.
11. Ni njia mojawapo ya kuwataarifu watu kuwa kuna hatari kwa hali hiyo wajihadhari.Sababu nyingine ni kuwa kipindi cha usiku kuna baadhi ya wadudu hatari kama vile nyoka, ambao wanafutiwa na sauti za miruzi.
12. Maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano na kuongezeka kwa utandawazi kumechochea zaidi mabadiliko yaliyopo katika jamii katika nyanja ya utamaduni.Mafunzo ya ugenini.
13. Yamechangia mambo mbalimbali kwa mfano, kuhamasisha vitendo viovu na vya kihuni kama vile ukahaba na ubakaji.
14. Ndio, Matumizi ya vyakula vya husaidia kujingika na maradhi mbalimbali, kujenga na kuimarisha virutubisho vya mwili
15. Tuweze kutambua, kuenzi na kuendeleza tamaduni zetu ambazo tumezirithi kutoka kwa mababu na bibi zetu ili kizazi kipya nacho kiweze kufaidika na tamaduni hizo.

## SARUFI

### SENTENSI ZA KISWAHILI

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuzitambua aina tatu za sentensi za Kiswahili.
2. Wanafunzi wazitaje sifa za kila aina ya sentensi kabla ya kutunga mifano ya sentensi hizi kwenye vitabu vyao kulingana na zoezi.
3. Mwalimu ahakiki kazi ya wanafunzi.

## KUANDIKA

1. Mwanafunzi aandike kisa juu ya utamaduni uliopitwa na wakati.
2. Mwanafunzi adhihirishe umuhimu wa utamaduni.Insha iwe ya mjadala.
3. Mwanafunzi atoe hoja zake za kupinga na kuunga mkono mjadala.
4. Mwanafunzi atoa hoja zake.
5. Insha iwe niya mjadala juu ya mbinu za kuhifadhi utamaduni.

# SURA YA 6: HAKI ZA BINADAMU

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

**Zoezi 1: Kazi ya vikundi**

1. Wanafunzi wataje baadhi ya haki wanazozijua.
2. Wanafunzi wataje jinsi ambavyo haki zao zimewahi hudhulumiwa.
3. Wanafunzi wataje jinsi ambavyo wamewahi kuwadhulumu wengine haki zao.
4. Wanafunzi watoe maoni na mapendekezo ya jinsi ya kurekebisha tabia na mitindo ya kudhulumu haki za wengine.

**Zoezi 2: Kazi ya vikundi**

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuzungumzia umuhimu wa haki za binadamu. Wanafunzi pia wazungumzie hali ya maisha inavyoweza kuwa iwapo haki za binadamu hazitiliwi maanani.
2. Wanafunzi wazungumzie wajibu wa serikali na jamii nzima kuhakikisha kwamba haki za raia hazidhulumiwi.
3. Wanafunzi wazungumzie wajibu wa wazazi kwa watoto wao. Wataje baadhi ya mambo wazazi hufawafanyia watoto wao kama wajibu wao.
4. Wanafinzi wasimuliane visa kuhusu haki zao.
5. Wanafunzi watazame picha na kusoma sentensi kuhusu haki za watoto. Kisha wafanye zoezi katika vutabu vyao.
6. Mwalimu ahakiki kazi ya wanafunzi. Wanafunzi waorodheshe haki na wajibu wa watoto na baadaye watunge sentensi wakitumia msamiati wa haki za watoto.

## KUSOMA

### HAKI ZA BINADAMU

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kusoma ufahamu. Wanafunzi wakitambue kichwa cha kifungu.
2. Wanafunzi wasome ufahamu kwa utaratibu wakizingatia mada ndogo zinazojitokeza katika ufahamu.

3. Baada ya kusoma ufahamu, wanafinzi wasimuliane kwa vikundi aina za haki walizozitambua kutokana na ufahamu.
4. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kuziorodhesha haki za binadamu.

**ZOEZI: JADILI**

**Haki za mtu aishiye na virusi vya ukimwi**

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kujadili jinsi wanvyoweza kuhakikisha kuwa haki za mtu aishiye na virusi vya UKIMWI zinatimizwa.

## SARUFI

**Kundi Nomino na Kundi Tenzi**

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kutofautisha kati ya kundi nomin na kundi tenzi.
2. Wanafunzi wataje aina ya maneno yanayotumiwa kuunda kundi nomino nay ale yanayounda kundi tenzi.
3. Wanfunzi wasome mifano ya sentensi wakitambulisha kunsi nomino na kundi tenzi.
4. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kufanya zoezi. Wanafunzi wakamilishe zoezi katika vitabu vyao.
5. Mwalimu ahakiki kazi ya wanafunzi.

## KUANDIKA

1. Mwalimu awaongoze wanafunzi katika kujadili kauli ya "Kumwajiri mtoto ni kumdhulumu".
2. Mwalimu asahihishe insha za wanafunzi. Mwalimu azingatie kuwa kiishio kilichopewa kimetumika. Mwalimu pia azingatie uakifishaji, matumizi ya msamiati mwafaka, utunzi bora wa sentensi na uwiano wa mawazo kwenya insha.